



ٲولٲى كى كٲارى؟ (Swahili)

UJANA? WAKO UMEUTUMIAJE ?



Yaliyowasilishwa Na
Majlis **Al-Madina-tul-'Ilmiyyah**

Kutafsiriwa Katika Kiingereza Na
Majlis-e-Tarajim (Dawat-e-Islami)

جوانی کیسے گذاریں؟

Jawani kaysay Guzarayn?

UJANA WAKO UMEUTUMIAJE?

Shaykh-e-Amir-e-Ahl-e-Sunnat, muasisi wa Dawat-e-Islami, ‘Allamah Maulana Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi داعية بَرَكَاتِهِمُ الْعَالِيَةِ alitua hotuba juu ya mada ‘*Jawani ki ‘Ibadat kay Fazail*’, i.e. *Excellence of Worship in Youth*, katika lugha ya Ki Urdu katika mjumuiko wa kila wiki wa Ijtimai ya kuhamasisha Sunnah iliyofanywa siku Alkhamis, 18th Rabi’-ul-Awwal 1412 AH, 26th September 1991, katika Markaz ya kwanza ya Dawat-e-Islami – ‘Jami’ Masjid Gulzar-e-abib’ (uliopo Gulistan-e-Okarvi Bab-ul-Madinah, Karachi). Kwa msaada wa hotuba hiyo hiyo, kijitabu pamoja na matoleo mengi na marekibisho kadhaa, kilikusanywa na Majlis Al-Madina-tul-‘Ilmiyyah in Urdu na kutafsiriwa na Majlis-e-Tarajim (idara ya tafsiri) kwa Kiswahili. Ikiwa utapata makosa katika tafsiri au utunzi, tafadhali ijuilishe idara ya tafsiri kwa anuani zifuatazo za posta au E.mail kwa azma ya kupata zawadi [Thawab].

Majlis-e-Tarājim (Dawat-e-Islami)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran,
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 1262

Email: ✉ translation@dawateislami.net

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.
Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَأَنْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf, vol. I, pp. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

Table of Contents

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu..... ii

Ujana Wako Umeutumiaje? 1

Fadhila za Darood Shariff.....	1
Kutafuta Ujana.....	2
Jibu la mawe mjibu kwa maua.....	4
Eneza kuwaalika watu kwa ajili ya Daawa njema.....	5
Uthamini hazina ya wakati wako.....	5
Sifa za ujana.....	6
Fadhila za Qur'an na ujana.....	7
Ibada ya ujana inakuwa sababu ya afya uzeeni.....	8
Madrassa ya watu wazima (Madrassa-tul-Balighan).....	8
Madrassa-tul-Madinah Balighat (Madrassa kwa ajili ya kina mama).....	9
Mazingira ya Dawat-e-Islami imemfanya mja mbaya kuwa mwema.....	9
Ni Neema ukiuthamini ujana.....	10
Uthamini ujana wako.....	11
Maagizo ya Sayyidunā Amīr Mu'āwiyah.....	12
Unyenyekevu wa wazee wetu ni mafunzo kwetu.....	12
Kwa baraka ya Ibada, Mzee huonekana kijana.....	13

Kufanya kazi ujanani ni faida uzeeni	14
Kijana mwema hupata zawadi yake uzeeni.....	14
Mja mpendwa wa Allah	15
Nani bora kuliko Malaika?	16
Kijana na Dawat-e-Islami	17
Mwenye kupata thawabu ya Sidiqeen Sabini (70)	19
Mja wa Mwenyezi Mungu wa hakika	19
Kijana mwenye kuona haya	20
Kupata ujana ni neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu.....	21
Fadhila za kijana mwenye kufanya Ibada.....	22
Fadhila za uzee	23
Kijana mwema anavyo pata zawadi	26
Karama za vijana.....	27
Kijana mwema na mwenye hofu.	29
Wale wenye kupata kivuli cha arshi.....	30
Usia wa Imaam Ghazali	32
Fadhila za kutubu ungali kijana.....	33
Kwanini anapendwa kijana mwenye kutubu katika ujana	33
Utubu kwenye ujana	34
Wasiwasi pamoja na tiba yake	35
Usia kwa ajili ya vijana.....	35
Madani Chanel ni nini?	37
Kwa niaba ya herufi 12 za kuingia na kutoka nyumbani ni maua i2 ya madani:.....	39

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Ujana Wako Umeutumiaje?



Shetani atatumia kila hila ili kukuzuia kusoma kitabu hiki, lakini utaingiwa na hofu ya Allah عَزَّوَجَلَّ kubwa baada ya kukisoma إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ.

Fadhila za Darood Shariff

Nabii wa Rehma Shafii wa Umaa Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema: ‘Enyi watu hapana shaka kati yenu ninyi yule mja aliyeniswaliya kwa wingi duniaini siku ya Qiama atafanyiwa hesabu yake haraka. (Jam’-ul-Jawāmi’, vol. 9, pp. 129, Ḥadīṣ 27686)

Ḥashr kī tīragī siyāhī mayn

Nūr ḥay, sham’-e-pur-ziyā ḥay Durūd

Ḥoḥiyo mat Durūd ko Kāfi

Rāḥ-e-Jannat kā raḥnumā ḥay Durūd

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Kutafuta Ujana

Inasemekana kuwa alikuwepo Mzee moja alikuwa anapita sehemu moja, kwa ajili ya uzee wake kiuno chake kilipinda wakati alipokuwa akitembea ilikuwa inaonekana kuwa huyu Mzee anatafuta kitu ardhini, kijana moja alimfanyia mzaha na kusema ‘Ewe Mzee unatafuta nini?’ Swali aliyeuiliza lilikuwa la kutia hasira lakini angalia huyu Mzee alivyo tumia hekima na busara na kumjibu swali liliyo kuwa na uchungu na alivyo mjibu kiutamu kwa kusema: ‘Mwanangu mimi nina tafuta ujana wangu’ Kijana alistajabu sana kusikia jibu na kushangaa na kusema ‘Baba neno lako hili sijaelewa, kwani ujana unaweza kuutafuta?’

‘Na lini ikiwa mara moja ujana ukikupotea kuna yeyote yule akaupata?’ Akasema ‘Mwanangu hapo ndio masikitiko yenyewe, wakati nilipo kuwa na neema ya ujana wangu sikuweza kuuthamini, nimeunawa mikono lakini leo nina jua umuhimu wake laiti ningepata mara moja enzi ya ujana wangu tena basi makosa niliyo yafanya na dhambi nilizofanya ningeweza kutubu na kufanya Ibada ya Allah عَزَّوَجَلَّ kwa moyo’.

أَلَا لَيْتَ الشَّبَابَ يَعُودُ يَوْمًا فَأُخْبِرُهُ بِمَا فَعَلَ الْمَشِيبُ

‘Maana yake laiti ujana wangu ungerudi na mimi ningeweza kumwambia uzee umenifanya nini na mimi’. Na kisha akavuta pumzi ya masikitiko na kusema: ‘Nasikitika nasikitika hazina

ya ujana wangu nimeipoteza, sasa ninasikitika! Wakati ndege wameshakula mazao na kuruka. Mimi sikuuthamini ujana wangu wakati ule wa ujana wangu sikufanya amali njema wala sikuji tayarisha kwa ajili ya akhera na hivyo ndio nime baki kwenye usingizi na kughafilika’.

‘Wakati Uzee umenijia, afya imepungua, ngozi imelegea lakini tamaa ya kufanya Ibada ninayo lakini siwezi kufanya kwa sababu ya uzee’.

Kisha yule Mzee mwenye makamo alimjaribu kumwambia yule kijana: ‘Mwanangu kwa fadhila ya Allah عَزَّوَجَلَّ na ukarimu wake wewe bado kijana chukua faida yake fanya Ibada kabla ya kiuno chako hakijapinda sujudu kwa Allah عَزَّوَجَلَّ kwa kupata ridhaa yake la siyoy usije ukawa kama mimi ukatafuta ujana na hutopata kitu chochote kile bali ni masikitiko na kujilaumu hakuna kitu chochote kitakacho kuja mikononi mwako, na utakuja kukumbuka. Utoto wako umeupoteza kwenye michezo, ujana wangu nimeupoteza kwenye usingizi, na hadi kufikia kwenye uzee hubaki kulia’. Maneno ya kijana huyo ya kumuumiza roho Mzee huyo wa makamo na Mzee alimpa usia na mazungumzo mazuri, alimpa kijana ua la Kimadani limeleta harufu nzuri kwa kijana na kumuingia ndani ya moyo na kuathirika, kijana huyu kabla ya mda mchache uliyo pita alimuliza swali la kumkashifu lakini kwa sababu ya huyu Mzee kujaribu kumpa nasaha nzuri na kijana huyu huyu aliahidi na kufanya nia mbele ya huyu Mzee ya kuwa atauthamini ujana wake na ataishi kuwa mwema.

Mwana wa A'lā Ḥaḍrat, Muftī-e-A'zam Hind Maulānā Mustafa Razā Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمٰنِ Ameandika shairi kuhusiana na ujana katika kitabu chake cha 'Saman-e-Bakhshish'

*Riyāzat kay yehī din ḥayn, buḥḥapay mayn kahān ḥimmat
Jo kuch kernā ḥo ab ker lo, abhī Nūrī jawān tum ḥo*

Siku za kufanya Ibada ni ujanani, ukifikia uzeeni hutoweza. Unachotaka kufanya ufanye ukiwa bado kijana.

أَمِينٌ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Jibu la mawe mjibu kwa maua

Wapenzi Waislaam! Baada ya kusikia Bayaan yenye hekima na Maua ya Kimadani, tutazungumzia ua moja la Kimadani nalo ni hili: Kama mtu anazungumza na wewe kwa ukali, mfano kakurushia jive na wewe badala yakumrushia jive uwe mstahamilifu na kisha ukipata nafasi umlinganie kwa upole na kumfahmisha na umpe nasaha na maua ya Kimadani إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ, italeta faida na isitoshe italeta ufanisi kwa ajili ya kazi za Kimadani na italeta mabadiliko kiwepesi ya azma yetu ya kuwa: nita jaribu kusuluhisha nafsi yangu na nafsi za walimwengu. Usirudi nyuma ewe mubaligh kila shambulio la shetani lisifaulu.

*Tū pīchay na ḥainā kabhī ay piyāray Muballigh
Shayṭān kay ḥer wār ko nākām banā day*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Eneza kuwaalika watu kwa ajili ya Daawa njema

Wapenzi Waislaam: Kutokana na kisa tulicho kisikia tumepata kujua maua ya Kimadani kuwa ujaribu kuwafahamisha Waislaam na uwaalike kwa ajili ya daawa njema. Na uwe unaendelea kuwaalika watu kwa ajili ya daawa njema kwa sababu inapatikana kheri yako na unaye mualika. Katika Aya ya Suratul Dhariaat no 55 Allah عَزَّوَجَلَّ anasema:

وَذَكِّرْ فَإِنَّ الذِّكْرَى تَنْفَعُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٥﴾

Tafsir: Wafahamishe kufahamisha kwako itawapa faida

Waislaam. Amesema Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Mujhāy tum aysī do hīmmat Āqā

Dūn sab ko naykī kī da'wat Āqā

Banā do mujh ko bhī nayk khaṣlat

Nabī-e-Raḥmat, Shaft'-e-Ummat

unipe hekima, niweze kuwaalika kwa ajili ya daawa njema.

Unipe hidaya ya kuwa mwema Nabii wa Rehma Shafii wa umma

Uthamini hazina ya wakati wako.

Kutokana na hikaya hiyo tumepata kuelewa kuwa tusipouthamini wakati wetu basi tutajilaumu siku za mwisho hasa tukija kuupoteza ujana wetu kwa kudharau tutakuja kujua umuhimu wake

tukifika kwenye uzee, kwa sababu safari yetu ya ujana tunaipoteza kwa kughafilika tutapofikia uzeeni na tunapotaka kubadilisha mwenendo wetu tunakuwa tumechelewa sana na mda huo mtu hutaka kufanya jambo lolote la kheri lakini mwili wake na viungo vyake pamoja na afya yake havimruhusu. Kwa hiyo kama umejaliwa neema ya ujana wako na afya yako ipo salama basi ushukuru na ufanye Ibada nyingi zaidi na utumie ujana wako kwenye kazi njema na ujaribu kuwa na istiqama na kama leo ukijighafilisha na ukapenda maslahi ya dunia na ukapoteza muda wako muhimu usije kesho ukasikitika, lakini kusikitika kwako hakutokusaidia kwa muda huo kwani hutopata kitu chochote mkononi mwako.

Mda ni kama mfano wa panga kali ambalo linakata usiku na mchana. Nani aliyeweza kuukamata muda mkononi mwake na nani anaweza kusema muda uende taratibu kwa hiyo leo chukua faida ya wakati wako la sivyo wakati uliyopita hautorudi tena bali utakumbuka tu .

Sadā ‘aysh daurān dikhātā nahīn

Gayā waqt phir hāth ātā nahīn

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Sifa za ujana

Kitengo kimoja cha Dawat-e-Islami Maktaba-tul-Madinah kimechapa kitabu kiitwacho Faizan-e-Sunnat chenye ukurasa

1548 jarida la kwanza ukurasa wa 713 kutokana na kitabu kimoja cha lugha kimeandikwa kuhusiana na mtoto anapoanza kubalehe na kufikia miaka 30 / 40 huitwa kijana na kuanzia miaka 30 / 50 unaumaliza ujana na kuingia uzeeni.

Fadhila za Qur'an na ujana

Wapenzi Waislaam: Unaweza kuchukua faida ya akili yako na mwili wako ungali kijana, kwa ajili ya mafunzo ya elimu ya dini na kufanya mtaala wa vitabu unatakiwa uwe kijana kwa sababu unapofikia uzee saa nyingine akili haifanyi kazi na saa nyingine akili huwa kama ya mtoto na saa nyingine ukifanya jambo watu wakikuona wanakucheka, lakini kuna habari nzuri kwa yule kijana aliye kuwa na mazoea ya kusoma Qur'an kwenye ujana wake akifika kwenye uzee hapati shida kama hizo. Jinsi anavyotueleza Sayyidunā 'Ikrimah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ Ananukuu Ḥakīm-ul-Ummat Muftī Aḥmad Yār Khān Na'imī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْعَظِيمِ anasema yule mUislamu aliye na mazoea ya kusoma Qur'an إِنَّ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ hatoathirika yaani afikapo uzeeni basi hatu kuwa na maradhi hayo. (*Nūr-ul-'Irfān, part 17, Surah Al-Hajj, Taḥt-al-Āyah 5*)

Filmaun say dirāmaun say day nafrat Tū Ilāhī!

Bas shauq mujhay Na'at-o-Tilāwat kā Khudā day

*Unijaliye chuki na picha na maonyesho
unipe mahaba ya qasida na kusoma qur'an mola*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ibada ya ujana inakuwa sababu ya afya uzeeni.

Wapenzi Waislaamu baada ya kusikia kisa hicho hapo juu tumepata kujua yule kijana mwenye kusoma Qur'an na akafika kwenye uzee basi kwa Baraka ya kusoma Qur'an hatoweza kupoteza ufahamu wake na hayo japo tunaweza kuona, kawida wazee wanapofikia umri huwa na ugonjwa wa kusahau lakini wale baadhi wenye bahati nzuri hata kama wakifika kwenye umri wa uzee bado fahamu yao na akili zao zinakuwa timamu. Hayo yote ni kwa sababu ya Baraka ya kusoma Qur'an kwenye ujana.

Madrassa ya watu wazima (Madrassa-tul-Balighan)

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Katika mazingira ya Dawat-e-Islami (taasisi ya kimataifa ya kueneza mafundisho ya qur'an na sunna isiyo jihusisha na siasa) Dawat-e-Islami ina jaribu kuhamasisha na kuwapa mafunzo ya kusoma Qur'an na kufundisha utaratibu wa Ibada, pia tuna kitengo kimoja kinachoitwa Madrassatul Balighan (Madressa ya Watu Wazima) ambayo ipo sehemu mbali mbali za Ulimwengu na katika maeneo mbali mbali hata hufundishwa msikitini. Kawaida huanza kufundisha baada ya swala ya ishaa ambapo sehemu karibu ya elfu moja hufundishwa ambao ndugu zetu Waislaam mubaligh, wana fundisha jinsi ya kusoma Qur'an kwa Makharij inavyo takiwa na wanatukumbusha Dua mbali mbali na pia kutufundisha jinsi ya kuswali inavyopaswa. Hayo mafunzo yote hufundishwa bure.

*Yeh̄i h̄ay ārzū ta'līm-e-Quran ām h̄o jāye
Ĥar aik parcham say aūnchā parcham-e-Islam h̄o jāye*

Madrassa-tul-Madinah Balighat (Madrassa kwa ajili ya kina mama)

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Katika mazingira ya Dawat-e-Islami tunacho kitengo cha akina mama wenye umri mkubwa ambayo ni Madrassa-tul-Madinah Balighat ambayo maelfu ya akina mama wanapata kujifunza kusoma Qur'an kwa makharij sahihi bure. Mafunzo hayo hufundishwa na mwanamke mwenzao na pia Madrassa ya kina mama zipo takribani kila mahala ulimwenguni.

Katika Nchi ya Pakistan zipo Madressa zifikazo 2064 ambapo wako wanafunzi wafikao 101,410 wavulana kwa wasichana ambao wanafundishwa bure kuhifadhi Qur'an.

*'Aṭā ḥo shauq Maulā Madrasay mayn ānay jānay kā
Khudāyā zauq day Quran paṛhnay kā, paṛhānay kā*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Mazingira ya Dawat-e-Islami imemfanya mja mbaya kuwa mwema

Madrassa ya Dawat-e-Islami Madrassa-tul-Balighan imemrahisishia kijana kwa ajili ya kusoma Qur'an na kumfundisha tabia njema na kumfanya awe na upendo wa kufanya Ibada ama kuchukulia hivi imemrahisishia kutengeneza akhera yake kuwa nyepesi. Kuna ndugu moja MUislamu anasema 'Dhambi zangu ni nyingi sana (mungu aninusuru) kazi yangu ilikuwa kusambaza

mtandao wa runinga na kukaa na kutembea na wahuni na kuenda kuangalia picha tatu kwa pamoja na kurudi usiku wamanane na pia kuangalia maonesho'

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Katika eneo moja la Bab-ul-Madina Karachi upande wa Naya Abaad, kwa baraka ya kuniling'ania ndugu mmoja wa kiislamu nimeweza kufika kwenye Madrastaul Baalighan na kukaa na wapenzi wa Mtume na kujumuika na mazingira ya Daawaat e islami. Na kujishughulisha na kazi za Kimadani.

Ĥayn Islāmī bhāī sabhī bhāī bhāī
Ĥay bayhad mahabbat bhārā Madanī Māḥaul

Ni Neema ukiuthamini ujana

Kuna riwaya kutoka kwa Sayyidunā 'Amr Bin Maymūn Awdī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ Mfalme wa Makka na Madina Nabii wa rehma shafii wa umma alikuwa anamsihi kijana mmoja. Alisema 'Unatakiwa uthamini vitu 5 kabla ya vitu 5 vikufikie:

1. Ujana wako kabla ya uzee
2. Afya yako kabla ya ugonjwa
3. Utajiri wako kabla ya umaskini
4. Wasaa wako kabla ya kushughulika kwako

5. Uhai kabla kifo. (*Mishkāt-ul-Maṣābīh, Kitāb-ur-Raqāq, chapter 2, vol. 2, pp. 245, Ḥadīṣ 5174*)

Mashoor sufi Sayyidunā Shaykh Muṣliḥuddīn Sa'dī Shīrāzī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْهَادِي anasema:

كُنُوتُ كِه دَسْتَسْت خَارِي بُكُنْ دِگَر كِي بَرَّارِي تُو دَسْتِ اَز كَفَن

“Ewe mja uliyeghafilika wakati una siha na afya na mikono yako iko wazi fanya kazi njema na mikono yako kesho ikija kufungwa ndani ya sanda utapata wapi bahati ya kuifungua!”
(*Būstān-e-Sa'dī, Bāb 1, pp. 48*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Uthamini ujana wako

Kuhusiana na ujana anasema Ḥakīm-ul-Ummat Muftī Aḥmad Yār Khān Na'imī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَنِي ameandika na amefafanua kwamba ujana umeupoteza kwenye michezo wakati ulipo fikia uzee viungo havifanyi kazi na kuweka tamaa ya kufanya Ibada ni upumbavu. Unacho taka ufanye kwenye ujana Ibada kwa vile ina daraja kubwa, kwa hiyo afya yako, ujana wako, pesa zako usiache zipotee ufanye amali njema nema hiyo haiji kila mara. Miyān Muhammad Bakhsh عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى Anasema:

Sadā na ḥusn jawānī raḥandī, sadā na suḥbat-e-yārān

Sadā na bulbul bāghān bolay, sadā na bāgh bahārān

Maana Ujana wako mzuri hautobaki salama milele, wala hautobaki uhusiano na marafiki na ndugu zako milele, na ndege wanayo imba pamoja na bustani iliyo kuwa nzuri haitobaki. (*Mirāt-ul-Manājīh, vol. 7, pp. 16*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Maagizo ya Sayyidunā Amīr Mu'āwiyāh

Anasema wakati wake wa mwisho wa uhai wake ulipokaribia kumalizika akasema “Nikalisheni” Wakati alipokalishwa yeye رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alijishughulisha kumdhukuru Mwenyezi Mungu na kulia nakujiuliza, “Ewe Mu'āwiyāh (رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ) sasa ulipofikia uzee ndipo umekumbuka kufanya dhikri ya Mwenyezi Mungu wakati ule ulikuwa wapi ingali bado matawi yalikuwa mabichi”. (*Lubāb-ul-Ihyā, pp. 352*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Unyenyekevu wa wazee wetu ni mafunzo kwetu

Ndugu Wapenzi Waislaam: Wazee wetu رَحْمَتُهُمُ اللهُ تَعَالَى walikuwa wema na wanyenyekevu. Masahaba wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Pamoja kuwa Masahaba watukufu maisha yao yote walikuwa wanafanya amali njema pia walikuwa wanasikitika kuwa laiti wangepata bahati ya nafasi zaidi wangepanya Ibada zaidi. Kwa kusikia ombi lao sisi tunapata muongozo kuwa: Enyi vijana, ni neema kubwa ungali kijana uthamini ujana wako usijighafilishe

na mambo yasiyo ya kheri la sivyo utaposhtuka itakuwa umechelewa sana sawa na mshale uliotoka kwenye upinde haurudi tena.

غَافِلٌ مِّنْشَيْئٍ نَّهٍ وَقْتُ بَازِي سِتٍ وَقْتُ هُنْرًا سِتٍ وَ كَارَسَايِ سِتٍ

Maana: Ewe kijana usikae bure, wakati huu sio wa wasaa wa kujighafilisha, bali wakati huu utumie kujifundisha na ufundi na uweze kufanya kazi.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Kwa baraka ya Ibada, Mzee huonekana kijana

Sayyidunā ‘Allāmah Ibn Rajab Ḥanbalī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِي Anasema kuhusiana na Ibada ya ujana: Yule mwenye kumkumbuka Allah عَزَّوَجَلَّ Kwenye ujana wake Allah عَزَّوَجَلَّ atamkumbuka wakati akiwa Mzee na hajiwezi na atamjalilia fahamu nzuri na nguvu. Sayyidunā Abū Ṭayyib Ṭabarī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِي aliishi zaidi ya miaka mia (100) na alikuwa mwenye afya na akili timamu. Mja mmoja alimuliza yeye عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى siri ya afya yake, yeye عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى Akasema: ‘Mimi kwenye ujana wangu nilihifadhi viungo vyangu na dhambi na leo mimi nimekuwa Mzee basi Allah عَزَّوَجَلَّ amenirejeshea nguvu zangu’. Alikuwa Mzee mmoja mwingine mwenye makamo hivyo hivyo Sayyidunā Junayd عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى Anasema ‘Nilimkuta Mzee moja anatembea kwa watu na kuomba omba, yeye عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى

anasema huyu kwenye ujana wake hakutumiza haki za Allah **عَزَّوَجَلَّ** na Allah **عَزَّوَجَلَّ** kwenye uzee wake amemuondolea nguvu zake'. (*Majmū'ah Rasāil Ibn Rajab, vol. 3, pp. 100*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Kufanya kazi ujanani ni faida uzeeni

Wapenzi Waislaam: Habari njema kwa yule kijana aliye tumia ujana wake kufanya Ibada ya Allah **عَزَّوَجَلَّ** hadi kufikia uzeeni, ambapo bado anatamani kufanya Ibada lakini mwili wake na nguvu yake haimruhusu basi **إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** ataandikiwa thawabu kama alivyo kuwa akifanya Ibada kwenye ujana wake. Na Sayyidunā Anas Bin Mālik **رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ** Anasema 'Wakati mja wa kiislaam anapofanya amali njema na akafikia kwenye dakika za mwisho za uhai wake basi Allah **عَزَّوَجَلَّ** humwandikia kwenye amali zake meema sawa sawa na meema aliyo kuwa akiyafanya kwenye ujana wake alipokuwa na afya'.

(*Musnad Abī Ya'la, vol. 3, pp. 293, Ḥadīṣ 3666*)

Kijana mwema hupata zawadi yake uzeeni.

Hakim-ul-Ummat Mufti Aḥmad Yār Khān **عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْكَرِيمِ** Anasema 'Yule aliye kuwa Mzee na hawezi kufanya Ibada zaidi kwa ajili ya uzee wake lakini kwenye ujana wake alifanya Ibada nyingi basi Allah **عَزَّوَجَلَّ** humchukulia ni mlemavu na kumwandikia thawabu kwenye amali yake iliyo kuwa sawa na ile aliyo kuwa akifanya Ibada kwenye ujana wake'.

رَسَمَ اسْتَكَيْه مَالِكَانَ تَحْرِيرِ
آزَاد كُنْتَدُ بَنْدَهُ پِيرِ
آءِ بَارِ خُدَا، آءِ عَالَمِ آرَا
بَرِّ سَعْدِي پِيرِ خُوْدَ بَهْ بَحْشَا

Kwahiyo uthamini ujana wako na ufanye Ibada zaidi na zaidi iwezekanavyo kwa sababu kesho ukiwa umefikia katika hali ya uzee na ukifanya Ibada utaandikiwa thawabu sawa ya ujana.

(*Mirāt-ul-Manājīh*, vol. 7, pp. 89)

صَلُّوْا عَلَيَّ الْحَبِيْبِ
صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيَّ مُحَمَّدٍ

Mja mpendwa wa Allah

Katika hadithi Kudsii: kuna riwaya kutoka kwa Sayyidunā ‘Abdullāh Bin ‘Umar رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا anasema Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema Allah عَزَّوَجَلَّ anasema yule mwenye kuleta imani juu yangu na ameridhika niliyomuandikia na mwenye kushukuru rizki niliyompa na kwa ajili ya ridhaa yangu matamanio ya nafsi yake ya kiwiliwili kaacha basi kijana huyu atakuwa kwenye ukumbi wangu pamoja na baadhi ya Malaika.

(*Jam’-ul-Jawāmi’*, vol. 9, pp. 276, Ḥadīṣ 28714)

Hakika! kama binadamu akiwa mwenye kumtii Allah عَزَّوَجَلَّ na akawa na mahaba na Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na akawa mtumwa wake kwa kujipenda basi daraja yake itakuwa sawa na Malaika na huenda akawazidi kwenye daraja.

Nani bora kuliko Malaika?

Wapenzi Waislaam: kumbuka kwamba Mtume wetu ni mbora kuliko mjumbe wa Malaika na mjumbe wa Malaika ni mbora kuliko Maauliya na Auliya ni bora kuliko Malaika wale wasio wajumbe na wale binadamu wanao tenda dhambi ni fasiq watawezaje kuwa bora kuliko Malaika. Kuna riwaya kutoka kwa. (*Fatāwā Razawīyah, vol. 29, pp. 391; An-Nibrās, pp. 595*)

Sayyidunā ‘Abdullāh Bin ‘Umar رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا anasema: Nabii wa Rehma Shafii wa Umma Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema ‘Mwenyezi Mungu atakuwa na mahaba na yule kijana ambae ujana wake ameufanyia waqfu kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ.’

(*Hilya-tul-Awliyā, vol. 5, pp. 394, Ḥadīṣ 7496*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wapenzi Waislaam; Bayaan mbili tulizozisikia hapo awali zina faida kubwa kwa yule atakaefuata maagizo yake, Yule kijana mwenye bahati nzuri atakae ishi kwa ajili ya ridhaa ya Allah عَزَّوَجَلَّ na akajiepusha na matamania mabaya na akajihifadhi na dhambi kwa ajili yake katika ukumbi wa Allah عَزَّوَجَلَّ kuna mategemeo ya kupata daraja kubwa, kwa sababu kipindi cha ujana kinakuwa na matamania mengi na huwezi kuyazuia ndio maana kuna fadhila kwenye Ibada ya ujana.

Kama jinsi Ḥakīm-ul-Ummat Muftī Aḥmad Yār Khān Na’īmī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْقَوِي anasema: Ujiepushe na dhambi katika ujana

wako na umkumbuke Allah عَزَّوَجَلَّ kwa sababu kwenye ujana viungo vinakuwa na nguvu zaidi na hukupeleka kwenye dhambi ndio maana Ibada ya ujana ni bora kuliko Ibada ya uzeeni.

(Mirāt-ul-Manājīh, vol. 1, pp. 435)

Wapenzi Waislaam: Leo kwa bahati mbaya sana vijana wako mbali na Qur'an na Sunna, na wamejighafilisha kwenye michezo kwa ajili ya matamanio ya nafsi zao wamezama na wanelea kwenye mto wa dhambi na wako mikononi mwa shetani na anasababisha watende dhambi. Tasisi ya Dawat-e-Islami isiyo jihusisha na siasa hufundisha Qur'an na Sunna inajaribu kuchukua jukumu la kuwaepusha kuzuia watu na kazi za kishetani.

Dawat-e-Islami ni kitabu kilicho wazi na inajulikana kwa kazi wanavyo fanya wale vijana waliyo kuwa wakifanya kazi za kishetani zisizokuwa za halali kwa ajili ya kuwa watumwa wa nafsi zao. Kwa bahati nzuri wamejumuika na mazingira ya Dawat-e-Islami yamewaitea mabadiliko kwenye maisha yao na ujana wao wakaufanyia waqfu kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ na Mtume wake صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Na kutimiza lengo la kuwa: ninatajaribu kurekebisha nafsi yangu na kusuluhisha nafsi za walimwengu mzima إِنَّ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ. Kijana na Dawat-e-Islami.

Kijana na Dawat-e-Islami

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Katika mazingira ya Dawat-e-Islami kuhusiana na mabadiliko mengi tutazungumzia jambo moja ambalo ni

muhimu sana. Vijana waliyo kuwa kwenye njia ya maovu imewabadilisha kuwa vijana wenye Taqwa, heshima na imewaonesha njia iliyo nyooka na imewatengenezea wenye kuwa na fikra ya Akhera. Kwa Baraka ya mazingira ya Dawat-e-Islami vijana wengi waliyo ghaflika na mambo ya dunia imewabadilisha wenye kuwa waqfu kwa ajili ya ridhaa ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Katika lugha ya Dawat-e-Islami tunasema: Waqf-e-Madinah.

*Maqbūl jahān bhār mayn hō Dawat-e-Islami
Ṣadaqaḥ tujḥay ay Rab-e-Ghaffār! Madīnay kā*

Siri ya maisha mazuri .

Wapenzi Waislaam: Nina ombi la Kimadani kwenu mtengeneze maisha yenu ya Dunia na Akhera na wakati wenu kuwa adhimu mjiunge na mazingira ya Dawat-e-Islami na mwenye kuinamisha mgongo kwa ajili ya Ibada ya Allah **عَزَّوَجَلَّ** na ni siri moja nzuri ya kufanya Ibada na kutii kama tulivyo amrisha kwa ajili ya maisha yetu.

Ḥakīm-ul-Ummat Muftī Aḥmad Yār Khān Naʿīmī **عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْقَوِي**
Anasema: Maisha ya kila binadamu yanapita, lakini maisha mazuri ni ya yule ambaye aliyekuwa waqfu kwa ajili ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. na kwajili ya watu kama hao. (*Tafsīr-e-Naʿīmī, vol. 3, pp. 134*)

Allah **عَزَّوَجَلَّ** Ametoa hukumu: ni sadaka kwao waliyo jitolea kuwa Waqfu kwa ajili yangu.

أَمِينٌ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Mwenye kupata thawabu ya Sidiqeen Sabini (70)

Kuna riwaya kutoka kwa Sayyidunā Anas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ anasema: Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Anasema: jiepushe na vitu aliyeharamisha Allah عَزَّوَجَلَّ Na wale vijana watakao tekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu basi watapata thawabu usawa wa Masidiqeen sabini. (*Attarghīb fī Faḍāil-ul-A'māl*, pp. 78)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Mja wa Mwenyezi Mungu wa hakika

Sayyidunā 'Abdullāh Bin Mas'ūd رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ anasema: Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema: Allah عَزَّوَجَلَّ Katika makhluk yake anampenda zaidi yule kijana ambae ujana wake na uzuri wake ameutumia kwa ajili ya Ibada ya Allah عَزَّوَجَلَّ Na Allah عَزَّوَجَلَّ Humsifia na kumdhukuru mbele ya Malaika na kusema huyu ni mja wangu wa hakika. (*Attarghīb fī Faḍāil-ul-A'māl*, pp. 78)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wapenzi Waislaam: Watakuwa vijana wenye bahati walio pata nafasi kwenye ukumbi wa Mwenyezi Mungu na upendo kwa wale waliotumia ujana wao kwa ajili ya kupata radhi ya Mwenyezi Mungu na wameacha matamaniao yao kwa kumwogopa Mwenyezi Mungu na wamekwepa mitego ya Shetani. Kwa ajili ya vijana kama hao wana habari njema kwenye riwaya tuliyoisikia hapo juu na vijana kama hao wanaheshimika duniani.

Kijana mwenye kuona haya

Ili kuwa kijana mwema na mwenye kuepuka dhambi na kuona haya (AIBU) ununuwe kitabu kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madina kinachoitwa *kijana mwenyekuona haya* au C/D iliyo rekodiwa na Maktaba-tul-Madinah uisome wewe mwenyewe na kisha umpatie mwenzio kuisoma na kuangalia **إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** utapata baraka na faida. Vijana waache maovu na wafuate maamrisho ya wazee na kuhudumia dini ya Kiislam kama shairi linavyo sema:

Tayray şofay ĥayn afrangī, tayray qālīn ĥayn Irani

Lāhū mujĥ ko rulātī ĥay jawāno kī tan āsānī

Amārat kyā, shakh-e-khusraw bhī ĥo to kyā ĥāşil

Nā zaur-e-Ĥaydarī tujĥ mayn, nā istighnāye Salmānī

Nā dhūnd is chīz ko tahzīb-e-ĥāzīr kī tajallī mayn

Kay pāyā mayn nay istighnā mayn mi' rāj-e-Musalmānī

Fanicha zako ni za Kingereza na mazulia yako ni ya Iran na mimi kuona maisha yako hayo machozi yananitoka. Hata kama wewe ukipata ufalme bado huna tabia njema na nguvu kama mola alivyo taka, pia huna mali kama Hadharat Salman Farsi, kama wewe unataka mema katika zama hiyo basi utoe sadaka nyingi.

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّد

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيب

Kupata ujana ni neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu

Wapenzi Waislaam: Kupata ujana ni neema kubwa ya Allah **عَزَّوَجَلَّ** Yule aliyebahatika kupata neema hiyo basi aithamini na kila ikiwezekana afanye Ibada zaidi wakati wake auchukulie kama thamani ya almasi usipotee bure, Ḥakīm-ul-Ummat Muftī Aḥmad Yār Khān **عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْعَالَمِينَ** ananukuu: Ibada ya ujana ni bora kuliko Ibada ya uzee kwavile mda haswa wa Ibada ni wakati wa ujana.

*Ker jawānī mayn ‘ibādat, kāhīlī achchī nahīn
Jab buṛḥāpā ā gayā kuch̄ bāt ban peṛtī nahīn*

*Ḥay buṛḥāpā bhī ghanīmat jab jawānī ḥo chukī
Yeḥ buṛḥāpā bhī na ḥogā maut jis dam ā gayī*

Tafsiri ya shairi: fanya Ibada wakati wa ujana usiwe mvivu. Wakati ufikapo uzeeni hutoweza kufanya Ibada. Na ushukuru kama umefikia uzee basi pia usiache kufanya Ibada kwa sababu baada ya uzee kuna kifo. Uthamini mda wako na ujue ni neema kwako mda utakapoondoka hutoupata tena.

(Mirāt-ul-Manājīh, vol. 3, pp. 167)

Khusasan ukizingatia wakati wa ujana wako ni muhimu sana kwa sababu katika ujana viungo vinakuwa imara na nguvu sana ndio maana kufanya Ibada huchoki na utaona raha, ufikapo uzeeni raha hiyo hutobahatika kuipata na kwa mda huo hata kwenda msikitini itakuwa ni shida pia hutoweza

kuvumilia njaa na kiu tukiacha Saumu za nafila hata za faradhi nazo itakuwa shida kuzifunga na hakika Ibada ya kijana ina nafasi kubwa.

Fadhila za kijana mwenye kufanya Ibada

Kuna riwaya kutoka kwa Sayyidunā Anas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ Anasema: Blessed Prophet صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema: Kijana mwenye kufanya Ibada asubuhi atapata fadhila zaidi kuliko Mzee ataefanya Ibada uzeeni, mfano Watume: walivyo kuwa bora zaidi kuliko watu wote. (*Jam'-ul-Jawāmi'*, vol. 5, pp. 235, *Hādīš 14769*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wapenzi Waislaam kutokana na riwaya ya hapo juu tumepata kujua hakika kijana mwenye kufanya Ibada kwenye ujana wake ana fadhila nyingi kwa ajili yake, lakini kutokana na riwaya hii asije mtu akachukulia kuwa wazee hawana thamani, ndugu zangu sivyo hivi, kumbuka kwamba hayo ni maneno ya kitenzi, kwa ajili ya watu wenye umri mkubwa na wazee pia wanakuwa sawa sawa.

Katika uislaam inakatazwa kabisa kuwapeleka wazazi wetu sehemu wanapo lelewa wazee (old house). Katika uislam ni jambo moja zuri sana ya kuwa hatutofautishi baina ya mweusi na mweupe kila mwislamu aliyekuwa mkubwa wa umri anaheshima yake katika Uislamu na kwa ajili ya heshima yake ni lazima Waislaamu wamheshimu na kama unataka ufafanuzi zaidi basi usome kitabu kilicho chapishwa na kitengo cha

Dawat-e-Islami Heshima ya Waislaamu. Kwa ufupi katika Uislamu ukiwa kijana ama Mzee unaheshimika, kwa hiyo:

Fadhila za uzee

Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema: Usingo'e nywele nyeupe kwani ni nuru ya Mwislamu, na yule anaezeeka kwenye Uislamu Allah عَزَّوَجَلَّ kwa ajili yake atamuandikia wema na atamfutia dhambi zake na atampadishia daraja lake. Kuna riwaya kutoka kwa.

(Sunan Abī Dāwūd, Kitāb-ut-Tarajjul, vol. 4, pp. 115, Ḥadīš 4202)

Sayyidunā Ka'b Bin Murrah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ Anasema Nabii wa Rehma Shafii wa Umma Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Anasema: Yule aliye kuwa Mzee ndani ya Uislamu siku ya Qياما atakuwa nuru kwa ajili yake.

(Sunan-ut-Tirmizī, Faḍāil-ul-Jihād, vol. 3, pp. 237, Ḥadīš 1641)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Kwa hiyo yule Mwislaam mwenye umri mkubwa yaani Mzee asisononeke wala asihuzunike na asijilaumu.

Ḥay burhāpā bhī ghanīmat jab jawānī ho chukī

Yeh burhāpā bhī na hogā maut jis dam ā gayī

Katika maisha ya uhai wako ukaja kushtukia kwenye umri mkubwa basi usisononeke bali uichukulie ni neema kwako na

kama umeshtukia nyakati za asubuhi basi usisubiri jioni kutanda mnyenyekee Allah عَزَّوَجَلَّ kwa ajili ya ridhaa yake na uwe mwenye Taqwa na uwe na mategemeo juu yake na uwe na hofu yake na pia uelekee kwake na ukumbuke aya hii.

لَا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ ط

Kwa kuweka aya hii إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ

Tuwe na mategemeo kuwa tutapata hazina ya toba na tutaporudi tutakuwa watu wema.

Tafsiri ya shairi: Uwe na mategemeo kama huweki elimu yako itaisha hiyo ni nema moja kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya Waislaam. Na ukumbuke kwamba kwenye umri wowote ule hata kama ni wazee kwenye ukumbi wa Allah عَزَّوَجَلَّ wenye bahati wakipata saada ya kutubu basi watubu la sivyo wangapi wameshafika kwenye uzee lakini bado wanaendelea kucheza michezo aina mbali mbali na kufanya kazi za haramu na kujishughulisha kwa kusanya amali mbaya kwa ajili ya akhera. Ujana wake aliupoteza kwenye kujighafilisha na uzeeni hakujaliwa taufiq ya kufanya kheri na sasa atapata nafasi gani kutayarisha kutafuta kheri kwa ajili ya akhera?

Ker na pīrī mayn tū ghaflat ikhtiyār

Zindagī kā ab nahīn kuch i'tibār

Halq per h̄ay maut kay khanjar k̄ dh̄ār
Ker bas ab apnay ko murdaun mayn shumār

Aik din mernā h̄ay ākhir maut h̄ay
Ker lay jo kernā h̄ay ākhir maut h̄ay

Tafsiri ya shairi: Usifanye uvivu uzeeni. maisha yako hayana uhakika. Juu ya shingo yako kuna kisu cha mauti. wewe ujihesabie kwenye wafu. Siku moja utakufa fanya unayotaka kufanya hakika mauti utapata.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ
تَوَبُّوا إِلَى اللَّهِ أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ
صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wapenzi Waislaam: Inatupasa sisi tuuthamini ujana wetu la sivyo tutapofika kwenye uzee na tukasikitika lakini hukutotusaidia, kwa vile ukitaka kufanya mema lakini mwili hauna nguvu, unakumbuka ujana wako lakini ujana wako haurudi tena, umechoka na uzee lakini uzee pia hautaki kwenda, na wakati huo kusikitika kwako hakuna faida.

Jo ā kay na jāye woḥ buḥhāpā daykhā
Jo jā kay na āye woḥ jawānī daykhī

Wakati unapojiwa na uzee, Uzee hauondoki na ujana ukiondoka haurudi tena.

Wapenzi Waislaam: Hakika Ibada ya ujana ina faida nyingi. Yule mwenye kufanya Ibada kwenye ujana na akajiepusha na madhambi angalia fadhila anazozipata kwa Mwenyezi Mungu.

Kijana mwema anavyo pata zawadi

Kitengo kimoja cha Dawat-e-Islami cha kuchapa vitabu (Maktaba-tul-Madinah) kitabu chenye kurasa 56 *Karama za Faruq-e-Azam* katika ukurasa wa 24 karama ya Faruq-e-Azam.

Mshauri wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, Sayyidunā ‘Umar Fārūq-e-A’zam رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ Safari moja alienda kwenye kaburi la kijana mwema mwenye Taqwa na kusema: Ewe kijana niambie Mwenyezi Mungu alilokuahidi.

وَلَيْسَ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ جَنَّاتٍ

Tafsir: Na yule mwenye kusimama kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ Na akamuogopa kwa ajili yake atabarikiwa pepo mbili.

Ewe kijana niambie hali yako ikoje? Yule kijana mwema mwenye Taqwa alimwita yeye رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ. Kwa kumwita jina lake kwa sauti ndani ya kaburi lake na kumwambia kwa sauti kubwa mara mbili فَدَّ أَعْطَانِيَهُمَا رَبِّي عَزَّوَجَلَّ فِي الْجَنَّةِ Maana Mwenyezi Mungu amenijalia pepo mbili.

(Tārīkh-e-Madīnah Dimashq, vol. 45, pp. 450)

سُبْحَانَ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ! Kutokana na kisa hiki tumepata kujua yule atakaeishi duniani kwa kufanya amali njema na akasimama kufanya Ibada kwa kumogopa Allah عَزَّوَجَلَّ na akawa na hofu ya mola na pia akawa mwenye Taqwa basi kwa rehma ya Allah عَزَّوَجَلَّ atastahili kubarikiwa pepo mbili, kwa hiyo ujana wako uutumie kwenye kufanya amali njema na mwenye kuwa na Taqwa na ujiepushe na matamanio ya nafsi na kumbuka kwamba ujana wako, uzuri wako, na mali yako usijivunie hivyo ni vya kupita mara moja tu.

*Dh̄al jāye gī yeh̄ jawānī jis pay tujh̄ ko nāz h̄ay
Tū bajā lay chāh̄ay jitnā, chār din kā sāz h̄ay*

*Utamalizika ujana wako ambao unaojivunia, maisha ni
ya siku nne.*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wapenzi Waislaam: tupate kusikia kisa cha vijana wawili wanavyo tunukiwa na kutupa mwanga moyo wetu.

Karama za vijana

Sayyidunā Mālik Bin Dīnār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَفَّاءِ Anasema: Safari moja mimi nilipokuwa safarini nilisikia kiu sana ya maji na kuanza kutafuta na kufika karibu ya jabali, ghafla nikasikia sauti na nikafikiri kuwa ni mnyama mkubwa ambae ananifuata na mimi nikaanza kukimbia mara nikasikia sauti ikisema, ewe

binadamu hakuna kitu kama hicho unachowaza huyu ni mcha Mungu ambae amevuta pumzi kubwa na sauti yake ikasikika. Kisha mimi nilipogeuka nyuma nilimkuta kijana mmoja ana fanya Ibada, mimi nilimsalimia na kumueleza shida ya kiu niliyo nayo, kijana akaniambia ‘Ewe Malik (رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ)! katika sehemu hii kubwa hujapata hata tone moja ya maji’ na kisha kijana alisogelea jiwe moja na kuipiga teke na kusema: ‘Ninaapa kwa kudra yako ambayo unayoweza kukusanya mifupa na kuwapa uhai utujalie maji na kututosheleza’.

Ghafa yakaanza kutoka maji katika sehemu hiyo kama chemchem ya maji, mimi nilikunywa kiasi cha kunitosheleza na kumomba aniusie kitu ambacho kitanipa faida.

Kijana akasema: ‘Fanya Ibada peke yako kwenye ukimya Mwenyezi Mungu hata porini hatokuacha na kiu’ baada kusema hayo kijana alirudi kwenye njia yake.

(Ar-Rauḍ-ul-Fāiq, pp. 166, amended)

Mayrī zindagī bas Tayrī bandagī mayn

Ĥī ay kāsh! Guzray sadā Yā Ilāhī

Tafsiri ya shairi: ‘Yaa illahi maisha yangu niutumikie kwa ajili ya Ibada yako.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Kijana mwema na mwenye hofu.

Sayyidunā Zunnūn Miṣrī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِي Safari moja alienda Shaam, yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alipita karibu na bustani moja ya kijani kibichi ambacho kilikuwa kinapendeza mno na kumwona kijana moja aliye kuwa chini ya mti mmoja wenye matufaa na alikuwa amejishughulisha na kuswali, yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alitaka kuongea na kijana huyo pindi alipomaliza kuswali na kutoa salamu. Mimi nilijaribu kuongea nae lakini hakunijibu kwa maneno bali kaniandikia shairi juu ya ardhi isemayo:

مُنِعَ اللِّسَانَ مِنَ الْكَلَامِ لِأَنَّهُ كَهْفُ الْبَلَاءِ وَ جَالِبُ الْأَفَاتِ
فَإِذَا نَطَقْتَ فَكُنْ لِرَبِّكَ ذَاكِرًا لَا تَنْسَهُ وَأَحْمِدُهُ فِي الْحَالَاتِ

Maana yake: Ulimi nimezuia kuutumia kwa sababu ni chanzo cha kuzungumza upuzi na ikawa sababu ya kuleta balaa kwa hiyo ukitaka kuutumia basi utumie kwa ajili ya kumdhukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu na usikae kimya. Shairi la kijana lilingusa sana moyo na yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alianza kulia wakati alipoanza kutulia basi yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alimjibu kwa kumwadikia kwa kutumia kidole cha shahada:

وَمَا مِنْ كَاتِبٍ إِلَّا سَبِيلٌ وَ يُبْقِي الدَّهْرُ مَا كَتَبَتْ يَدَاهُ
فَلَا تَكْتُبْ بِكَفِّكَ غَيْرَ شَيْءٍ يَسْرُكُ فِي الْقِيَامَةِ أَنْ تَرَاهُ

Maana yake: Yule mwenye kuandika siku moja atakuja kufa lakini aliyo acha kwenye mandishi yatabaki milele kwa hiyo uandike kitu kizuri ili utakapo kuta siku ya Qiyama uifurahiye.

Sayyidunā Ẓunnūn Miṣrī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَظِيمِ Anasema: Kijana baada ya kusoma niliyoandika alipiga chafya moja na ndipo roho yake ilitoka hapo kwa papo na mimi nilibaki kuwaza na kutayarisha shughuli ya kumzika lakini ikasikika sauti ikisema mwache Ẓunnūn! Mwenyezi Mungu amemuahidi kuwa Malaika watamshughulikia habari za mazishi yake, baada kusikia hayo yeye عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى alienda kona moja ya bustani na kuendelea kufanya Ibada baada ya kumaliza rakaa kadhaa alipoangalia hakukuta kitu chochote wala alama haikuwepo.

(Rauḍ-ur-Riyāḥīn, pp. 49, amended)

Rahūn mast-o-bay-khud mayn Tayrī wilā mayn

Pilā jāṃ aysā pilā Yā Ilāhī

Tafsiri ya shairi: *Ilahii nakuomba uninyweshe maji ya mapenzi yako ambayo niweze kuwa majnoon kwa ajili yako.*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wale wenye kupata kivuli cha arshi.

Hongera kwa wale vijana walio kuwa na hofu na wakafanya Ibada ya Allah عَزَّوَجَلَّ siku ya qiyama jua litakapokuwa umbali wa maili moja na robo itakuwa hakuna kivuli cha aina yeyote

ile ila kivuli cha arshi na watu watahangaika kwa joto, watakuwa wana tapa tapa na majasho yatakuwa yanawatiririka basi siku hiyo patakuwa na kivuli cha arshi na wale vijana waswalehina wenye bahati watakuwa chini ya arshi hiyo.

Sayyidunā ‘Abdur Raḥmān Jalāluddīn Suyūṭī Shāfi’ī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْكَافِي amemuandikia barua Sayyidunā Salmān رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ amemuandikia barua Sayyidunā Abū Dardā رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ na kumweleza kuwa watu wawili pia watakuwa kwenye arshi hiyo ni:

1. Yule kijana ujana wake aliyetumia kwa ajili ya kumridhisha Allah عَزَّوَجَلَّ na.
2. Yule aliyefanya Dhikri ya Allah عَزَّوَجَلَّ na akatoa machozi kwa ajili yake.

(Muṣannaf Ibn Abī Shaybah, Kitāb-uz-Zuhd, vol. 8, pp. 179, Ḥadīṣ 12)

*Yā Rab mayn Tayray khauf say rotā raḥūn ḥer dam
Tū apnī maḥabbat mayn mujḥay mast banā day*

Tafsiri ya shairi: Yaarabi unijaliye mimi niwe ninalia kwa ajili ya hofu yako.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wazee wetu wacha Mungu jinsi gani walikuwa wakiuthamini ujana wao na wanatusisitiza kuuthamini ujana wetu.

Usia wa Imaam Ghazali

Ḥujjat-ul-Islam Sayyidunā Imām Abū Ḥāmid Muhammad Bin Muhammad Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْوَالِي Anasema kwa wale vijana wanao chelewesha kutubu wana ambiwa je hufikirii kuwa umejidanganya nafsi yako na kuahidi uongo kuwa utafanya amali nema kesho, hiyo kesho ikabadilika kuwa leo, je ungejua hiyo jana iliyokuja imeondoka? Na kesho yake ikaja kuwa na mabadiliko? Kwa hakika ukifanya amali leo kesho unaweza kufanya ziada. (Yule mwenye kuacha kazi yake ya kutwa na mwenye kuchelewa kutubu) yuko mfano wa yule mtu aliyetaka kung'oa mti katika ujana wake na aliuacha na akaja kuung'oa baada ya mwaka wakati alikuwa anajua kila mda unavyo kwenda mbele mti utakuwa mkubwa na mizizi itaenea mg'oaji nae nguvu zake zitapungua basi kama hakuweza kuung'oa wakati wa ujana basi atashindwa kuung'owa wakati wa uzee.

(Ihyā-ul-'Ulūm, vol. 4, pp. 72)

Tafsiri ya Shairi: *Fanya mema kwa wingi mfano wa mwezi unavyo waka na kadri unavyo pungua mwanga basi sawa na wewe umri wako pia unapungua.*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wapenzi Waislaam: Maneno mazuri ya Imām Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْوَالِي yanatupa fikra kama hukuzingatia sheria wakati wa ujana wako na wala hukufanya Ibada na ukaupuuza utategemea nini kwenye uzee wako kurekebisha makosa yako pindi viungo

vyako vimeshazee, kwa hiyo ufanye haraka na utubu kwa vile wakati wowote unaweza kuletewa taarifa ya kifo chako kwani kifo hakichagui kijana wala Mzee

Tafsiri ya shairi: *Kifo hakichagui kijana wala Mzee pia hakiangalii mwenye umri wa miaka 16 ama 55.*

Fadhila za kutubu ungali kijana

Mpendwa wa Mwenyezi Mungu Nabi wa Rehma Shafii wa Umma Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Anasema:

إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يُحِبُّ الشَّابَّ التَّائِبَ

maana yake: *Mwenyezi Mungu anampenda yule mja anae tubu kwenye ujana wake.*

(Kanz-ul-'Ummāl, Kitāb-ut-Taubāh, Al-Juz 4, vol. 3, pp. 87, Ḥadīṣ 10181)

Kwanini anapendwa kijana mwenye kutubu katika ujana

Mubaligh wa kislām 'Allāmah Shaykh Shu'ayb Ḥarīfīsh رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ anasema; Mwenyezi Mungu anampenda mja wake wakati ule yungali yeye ni kijana na kisha anatubu kwa sababu umri wa kijana unakuwa una nguvu mfano wa matawi mapana. Wakati ujana wake unamshawishi kwa kumletea ladha tofauti ya kila aina ya starehe lakini yeye huzikwepa na kutubu na wakati huo

kwake inakuwa dunia inavutia lakini kwa ajili ya ridhaa ya Allah ﷺ ana acha vitu vyote basi anakuwa mustahik wa Allah ﷺ na anawekwa pamoja na waja wake watukufu.

(*Hikāyatayn aur Naṣīhatayn*, pp. 75)

Kuna riwaya kutoka Kwa Sayyidunā Anas Bin Mālik رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ anasema: Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Anasema: Hakuna kitu zaidi anapenda kuliko kijana mwenye kutubu.

(*Kanz-ul-'Ummāl, Kitāb-ul-Mawā'iz, Al-Juz 15, vol. 8, pp. 332, Ḥadīṣ 43101*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Utubu kwenye ujana

Wapenzi Waislaam: Kijana anaefanya Ibada kwenye umri mdogo na anatubu anapata saada kuwa Allah ﷺ anapenda ni hakika.

دَر جَوَانِي تَوْبَهُ كَرْدَن شَيَوَهُ بِيغَمَبَرِي
وَقْتِ پِيرِي گُرگِ ظَالِمِ مِي شَوَد پَرهيزگار

Maana kufanya istighfar kwenye ujana ni sunna ya عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ Katika uzee hata mdhalimu pia anakuwa mtu mzuri anakuja kufunika shuka ya kuwa mtu mwenye taqwa.

Tafsiri Ya Shairi: Ni sunna ya ambiya kutubu kwenye ujana ufikapo kwenye uzee, hata mbwa mwitu huwa mwema.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wasiwasi pamoja na tiba yake

Unaweza ukawa na wasiwasi kwa kusikia shairi iliyo zungumzia hapo juu ya kuwa عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ Mungu atawanusuru je عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ wanaoweza kutenda dhambi?

Tiba ya wasiwasi: Haiwezekani haiwezekani kabisa عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ Hawakosei na hawana dhambi wao ni maasum, na maana ya Maasum wameshafanya ahadi na Mwenyezi Mungu kutokana na ahadi hiyo hawataweza kufanya dhambi ya aina yeyote ile kwa vile hiyo ni hakika kabisa ya kuwa عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ wote ni Masum na wameepuka na dhambi ndogo na kubwa na walikuwa Masum kabla ya kupata Utume na baada ya kupata Utume.

(Derived from: Bahār-e-Sharī'at, vol. 1, pp. 38-39)

Tafsiri ya shairi: Umbile la Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ halina kasoro Mtume wetu ni ua lisilo na miba Mtume wetu ni mwanga usio na moshi. Kuhusina kwa neno لا عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ kusema wame tubu ni kwa ajili yetu sisi kutuonyesha jinsi gani walivyo kuwa wapole na wanyeyekevu pamoja hawatendi dhambi lakini wanatuonyesha jinsi ya njia ya kumomba Allah عَزَّوَجَلَّ hayo yote ni mafundisho kwetu na ndio maana inaitwa sunna ya عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ مُحَمَّد

Usia kwa ajili ya vijana

Hujjat-ul-Islam Sayyidunā Imām Muhammad Bin Muhammad

Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْوَالِي Anasema: Sayyidunā Mansūr Bin ‘Ammār عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَقَّار! alimsihi kijana moja kwa kusema; Ewe kijana ujana wako usije ukakudanganya walikuwa vijana wangapi walio chelewesha kutubu na kujipa moyo na walisahau Mauti na kusema tutatubu kesho ama keshokutwa na kujighafilisha hadi Malakal Mauti amewasili na kuteremshwa kwenye kaburi lenye giza hakusaidiwa na mali zake, marafiki zake, watoto wake na wazazi wake.

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ ﴿٨٨﴾ إِلَّا مَنْ آتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ ﴿٨٩﴾

Maana !ya Aya: Siku hiyo haitokusaidia Mali yako wala watoto wako, Ila yule alofika Kwa Mwenyezi Mungu Na amali njema.

[Kanz-ul-Īmān (Translation of Quran)] (Part 19, Ash-Shu'arā, verses 88-89)

(Mukāshafa-tul-Qulūb, pp. 87)

Tafsiri ya shairi: Umande unasema uzuri wa dunia sio kitu na ndege wanasema maua yataisha na huo mwezi unaotumulika ni kwa ajili ya siku nne na baada ya hapo kuna giza ewe kijana uzuri wako na ujana wako utakuja kuisha .

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

تُؤَبُّوْا إِلَى اللَّهِ أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wapenzi Waislaam: Kwajili ya kutayarisha akhera, kuepuka na dhambi, kuwa na istiqama juu ya wema jiunge na mazingira ya Kimadani.

Kupata na kujifunza tabia za Sunna usafiri na wapenzi wa Mtume kwenye Madani Qafilah na kwa ajili ya kuishi maisha mazuri na kutengeneza akhera yako basi kila siku ujaze kadi ya Madani Inaamat na ifikapo kila mwisho wa mwezi mkabidhi muhusika na ujitahidi kuhudhuria Ijtimai ya kila wiki na uwe mwenye kutubu na upate istiqama na ukitaka kujua kwa kina kitengo cha uchapishaji wa vitabu Maktaba-tul-Madinah imechapa kitabu chenye ukurasa 132 kiitwacho *Toba na hikaya*.

Ukisome kupata elimu na hekima na mapenzi ya awali basi hudhuria na wale waliyokuwa nje ya Pakistan wanaweza kushiriki katika Madani Muzakara kupitia runinga kwenye Madani Channel.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Madani Chanel ni nini?

Idara ya uchapishaji wa vitabu Maktaba-tul-Madina imechapa kitabu cha madhara ya usengenyaji katika ukurasa wa 86.

!الْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ

Katika mazingira ya Dawat-e-Islami tasisi ya kimataifa ya kueneza mafundisho ya Qur'an na Sunna isiyojihusisha na siasa kutokana na kitengo chake kimoja cha Madani Chanel ambayo ina rusha mtandao wake takribani nchi nyingi, na inafikisha ujumbe wake kila nyumba. Madani Chanel ni mtandao wa peke yake duniani ambao asili mia inao onyesha habari za dini tu, haina matangazo, michezo ya kuigiza, muziki hata mwanamke haonyeshwi.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Kutokana na Madani Chanel makafiri wameingia kwenye Uislaamu na wenye kusali wamekuwa hawaachi hata sala moja na wengi wametubu dhambi yao na kuwa wenye kufuata sunna. Kwa baraka ya Madani Chanel ndugu moja wa kislaamu ameniandikia Email inasema hivi: Watu wanapo ongea maneno hawatambui kuwa wana sengenya kwa vile hawajui. Safari moja walitoka watu kutoka Haidra Baad Sind na kuelekea Bab-ul-Madinah Karachi, ndugu moja akasema mbele za watu rafiki zangu waliniambia kuwa dada yake ana tabia ya kuwa na hasira sana na akikasirika na yeyote yule basi hazungumzi nae, wifw yangu na dada yangu kwa jambo dogo dogo wanagombana na ndio maana haongei nae.

Bahati nzuri usiku ule katika Madani Chanel ilikuwa maada ya jinsi gani kuepuka na mambo za kusengenya. Dada yangu ambae aliye kuwa na hasira asiyetaka kuonana na mtu yeyote yule alipoona Madani Muzakra basi **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ** palepale aliinuka na kumwomba msamaha na kupatana tena.

Tafsiri Ya Shairi: Madani Chanel imeepuka na Muziki na Ngoma, na Chanel hii haiogopi kusema Ukweli. Katika Chanel hii inatufundisha Sunnah za Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, na Shetani hafurahii Chanel hiyo.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Wapenzi Waislaam: Ninamaliza Bayaan yangu kwa kueleza fadhila za Sunna na kuelezea Sunna kwa uchache. Nabii wa rehma shafii wa umma mfalme wa makkah na madina Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema: yule mwenye kuipenda sunna yangu basi kanipenda mimi na yule mwenye kunipenda mimi basi atakuwa pamoja na mimi peponi.

(Mishkāt-ul-Maṣābīh, vol. 1, pp. 55, Ḥadīṣ 175)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Kwa niaba ya herufi 12 za kuingia na kutoka nyumbani ni maua i2 ya madani:

1. Wakati ukitoka nyumbani usome Dua hiyo:

بِسْمِ اللَّهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ

Maana: Kwa jina la Allah عَزَّوَجَلَّ mimi nimemuamini Allah عَزَّوَجَلَّ bila ya jina lake Allah عَزَّوَجَلَّ Sina nguvu wala uwezo. إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ Kwa baraka ya kusoma dua hiyo utakuwa kwenye njia iliyo nyooka, utaepukana na balaa na utakaa kwenye hali nzuri. *(Sunan Abī Dāwūd, vol. 4, pp. 420, Ḥadīṣ 5095)*

2. Wakati ukiingia ndani ya nyumba usome dua hii:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَ الْمَوْلَجِ وَخَيْرَ الْمَخْرَجِ بِسْمِ اللَّهِ
وَلَجْنَا وَبِسْمِ اللَّهِ خَرَجْنَا وَعَلَى اللَّهِ رَبِّنَا تَوَكَّلْنَا

Maana: Mimi ninakuomba wewe kheri ya kuingia na kutoka nyumbani kwa jina lako Allah عَزَّوَجَلَّ Umeingia ndani kwa jina lake na umetoka nje kwa kumkabidhi yeye Allah عَزَّوَجَلَّ Baada ya kusoma dua hiyo uwasalimie watu wa nyumbani, kisha uende kwenye ukumbi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Na utoe salaam baada ya hapo usome إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ Sūrah Al-Ikhlās Utapata baraka kwenye riziki yako na utaepukana na ugomvi wa nyumbani.

(Sunan Abī Dāwūd, vol. 4, pp. 420, Ḥadīṣ 5095)

3. Unapoingia nyumbani kwako na kutoka wasalimie Maḥārim na Maḥrimāt (Mama, baba, dada, kaka, watoto na kadhalika)
4. Bila ya kutaja jina ya Allah عَزَّوَجَلَّ yaani بِسْمِ اللَّهِ, na ukaingia nyumbani kwako basi shetani ataingia pamoja na wewe.
5. Kama unaenda kwenye nyumba yako na hakuna watu basi usome hivi:

السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ

Maana yake ni salaam iwe juu yetu na kwa waja wema wa Allah ﷺ Malaika watajibu salaam hiyo ama utoe salaam kwa namna hiyo (*Rad-dul-Muhtār, vol. 9, pp. 682*)

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ

Maana yake (Mtume salaamu iwe juu yako) kwa sababu roho ya Mtume ﷺ Inakuwa hadhiri nyumba za Waislaamu. (*Sharah Ash-Shifā lil-Qārī, vol. 2, pp. 118*)

6. Kama unaenda nyumbani kwa mtu basi utoe salaamu kwa kusema hivi: **السَّلَامُ عَلَيْكُمْ!** Na umulize je mimi ninaweza kuja ndani?
7. Kama hujaidhiniwa basi urudi kwa furaha inawezekana kuwa ana udhuru fulani hajaweza kukupa ruksa ya kuingia ndani.
8. Kama mtu anabisha hodi nyumbani kwako basi ni sunna umulize wewe nani ? Yule aliyekuwepo nje ajitambulisha jina lake mfano aseme Mohammed Elyas. Badala ya kutaja jina ukasema Madina ni mimi fungua mlango ama kutamka neno jingine lisilo la kisunna.

9. Baada ukishamjibu kwa kutaja jina lako basi usogee mbali na mlango kwa sababu itapofunguliwa mlango usije ukaona mpaka ndani.
10. Kuchungulia nyumbani kwa mtu imekatazwa. Baadhi ya watu wanaoishi magorofani wanatakiwa wawe waangalifu sana kwa kuwa kuna watu wanaoishi nyumba za chini na pia nyumba inayotazamana mbele yake.
11. Kama unaenda nyumbani kwa mtu na kakutayarishia kitu usilaumu wala usimseme kwa vile atasononeka.
12. Wakati unapo rudi kutoka nyumbani kwa mtu basi mshukuru kwa maandalizi yake na umombee dua kwa ajili ya haki yake na umuage na ikiwezekana mpe zawadi ya risala nakadhalika.

Kwa kujifunza Sunna nyingi ununue kitabu kilicho chapishwa na Maktabatul madina Bahar-e-Shari'at chenye ukurasa 312. Katika ukurasa wa 120 *Sunna na Adabu* zake uisome. Na njia moja nzuri kwa ajili ya kujifunza Sunna na kupata tabia njema ujiunge na Dawat-e-Islami na usafiri na wapenzi wa Mtume katika Madani Qafilah.

Sīkh̄nay sunnatayn Qāfilay mayn chalo

Lūtnay rahmatayn Qāfilay mayn chalo

Ĥaun gī ḥal mushkilayn Qāfilay mayn chalo
Pāo gey barakatayn Qāfilay mayn chalo

Kujifunza sunna twende kwenye qafilah

Kupata rehma twende kwenye qafilah

Kutatua matatizo twende kwenye qafilah

Kupata baraka twende kwenye qafilah

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ
تُوبُوا إِلَى اللَّهِ أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ
صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ


Baraka Za Sunnah

Katika mazingira mazuri ya Dawat-e-Islami (Shirika la Kimataifa la Kueneza Mafundisho ya Quran na Sunna lisilojihusisha na siasa) sunna za Bwana Mtume **حَلِّ اَللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ** zinafunzwa kwa wingi.

Ni ombi kwa kila muislamu kuhudhuria na kukesha usiku mzima kwa nia ya kutaka radhi za Allah **عَزَّوَجَلَّ** pamoja na niya zingine nzuri katika ijtimai ya kila wiki siku ya Alhamisi baada ya sala ya Magharibi inayofanyika katika mji anaoshi. Vile vile ni ombi kwa kila muislamu kusafiri na wapenzi wa Mtume **حَلِّ اَللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ** katika Madani Qafila kwa nia ya kupata thawabu na kujifunza sunna za Bwana Mtume **حَلِّ اَللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ**. Na afanye Fikr-e-Madina (kujisaili mwenyewe) kwa kujaza kadi ya Madani In'amaat na amkabidhi Zimmedaar (msimamizi) wake katika siku kumi za mwanzo za kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivyo **اِنْ شَاءَ اللّٰهُ عَزَّوَجَلَّ** tutaweza kushikamana na sunnah za Mtume **حَلِّ اَللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ** na tutachukia maasi na tutazidi kuwa na hamu ya kulinda imani yetu.

Kila muislamu aweke azma ya kwamba: "Nitajaribu kusuluhisha nafsi yangu na watu wote wa ulimwengu mzima" **اِنْ شَاءَ اللّٰهُ عَزَّوَجَلَّ**

Kwa ajili ya kusuluhisha nafsi yangu nita fuata Madani In'amaat na kusuluhisha nafsi za watu wa ulimwengu nita safiri katika Madani Qafilah. **اِنْ شَاءَ اللّٰهُ عَزَّوَجَلَّ**



www.dawateislami.net



MC 1286

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan.

UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 1262

Web: www.dawateislami.net | E-mail: translation@dawateislami.net